

# Maswali

1. Nani alibaki hai baada ya gharika?.
2. Watu wote walinena lugha moja?
3. Watu walitaka kujenga nini?
4. Mnara ulikuwa uwe namna gani?
5. Walijifikiria namna gani?
6. Mbona BWANA alishuka chini.
7. Mungu alifikiri watu wanafanya nini?
8. Mungu alifanya nini?
9. Je hawa watu walimaliza kujenga mji?
10. Mji uliitwa je?

# Majibu

1. Baada ya gharika,Nuhu ,watoto wake (Shemu, Hamu na Yafethi) na wake wao walibaki hai.
2. Ndio watu wote walinena lugha moja.
3. Watu walitaka kujenga mji na mnara .
4. Mnara ungekuwa mrefu wa kufika mbinguni.
5. Watu walifikri wao wana akili na nguvu.
6. BWANA alishuka chini kuona walichokuwa wakifanya.
7. Mungu alifikiri kwamba watu walikuwa wamesahau kwamba ana uwezo.
8. Mungu aliwatawanyisha kisha akawafanya waongee lugha tofauti.
9. Mji haukumalizika.
10. Mji uliitwa Babeli.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

**Awamu ya 1 Mwaka wa 2**



## 1 Mnara wa Babeli

### Marejeo

Mwanzo 11

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba baada ya gharika watu walikuwa na shaka na nguvu za Mungu lakini yeye huangalia kila jambo na anauamuzi.

### Maneno maalum

1. Baada ya gharika +watu wengi+ lugha moja.
2. Jenga +mji+mnara +wenye akili
3. Bwana alishuka+watu walisahahu.
4. Badili lugha +watu kutawanyika
5. Simamisha ujenzi+Babeli.

**1.1** Baada ya gharika iliyoletwa na Mungu, Nuhu alibaki na jamii yake. Watoto wake walikuwa Shem, Hamu na Yafethi. Nao walikuwa na familia zao. Baadaye nchi ikawa na watu wengi na walizungumza lugha moja.

**1.2** Watu hao walipata mahali pakujenga mji. Walitengeneza matofali kutoka kwa udongo. Walitaka kujenga mnara mrefu, Mnara mrefu sana wakufika mbinguni. Walijitakia jina kubwa ili waendelee kukaa pamoja. Walifikiri kwamba wana akili na nguvu, tena ni wamaana sana.

**1.3** Walipokuwa wakijenga mnara BWANA alishuka ili aone wanafanya nini. Mungu alikadhabika kwa kuona watu wamesahau njia zake. Hawakukumbuka alivyo sema kwamba hataleta gharika ingine na yeye ni wauwezo .Akasema, "Hawa watu wanassema lugha moja na wanajipenda. Si muda watafikiri kufanya lolote na kunisahau."

**1.4** Mungu aliamua kuwakatisha wasifanye shauri za kutojali. Aliwatawanyisha kwa nchi nzima. Kukawa na lugha mpya tofauti. Hawakuelewana tena. Hawakufanya mashauri pamoja tena.

**1.5** Watu waliacha kujenga mji. Waliuita "Babeli" Maana yake "Chafua".

